

PALE MAHALI ANAPOKAA MUNGU

Waefeso 2:18-20 kwa maana kwa Yeye sisi sote tumepata njia ya kumkaribia baba kwa roho mmoja, Basi sasa ninyi si wageni wala wapitaji. Bali ninyi ni wenyeji pamoja na watakatifu watu wa nyumbani mwake Mungu. Mmejengwa juu ya msingi wa Mitume na Manabii, Naye Kristo Yesu mwenyewe ni jiwe kuu la pembeni katika Yeye jengo lote linaunganishwa vyema na kukua hata liwe hekalu takatifu katika Bwana. Katika yeye ninyi na ninyi mmejengwa pamoja kuwa maskani ya Mungu katika Roho .

Angalia wale walio na uzima wa milele walikua pamoja Naye na ndani Yake katika mawazo Yake, kabla hakujawahi kuwa na malaika nyota, kerubi au chochote kile. Hiyo ilikuwa ni milele na kama una uzima wa milele **(Yohana 5:24)**

Ulikuepo siku zote, sio utu wako hapa lakini sura yako na umbo lako ambalo Mungu asiye na kikomo.....

Sasa kama Yeye Ana kikomo atakuwa siyo Mungu .Mungu ni lazima awe na asiye na kikomo **(1Wafalme 8:27)** Sisi tuna kikomo, yeye hana kikomo.Yeye ni aliye kila mahali ni ajuaye kila kitu na asiyeshindwa na kitu. Kama yeye hayuko hivyo basi sasa hawezi kuwa Mungu , anajua mambo yote, anajua sehemu zote kwasababu ya kuwa kwake kila mahali. Kule kujua yote kutamfanya Yeye kuwa kila kila mahali, yeye ni kiumbe yeye si kama upepo yeye ni kiumbe. Ana kuwa katika nyumba **(Kutoka 25:40: Waebrania 8:1.5)** Lakini yeye akiwa anajua yote,Kujua vitu vyote kunamfanya yeye kuwa kila mahali kwa sababu anajua kila kitu ambacho kinaendelea hakuna kioboto ambaye atapepesa macho bila yeye kujua hilo na alilijua hilo kabla kuwepo ulimwengu ni mara ngapi kingepepesa macho yake, na ni mara kiasi gani ulikuwa ndani yake huyo ni asiye na kikomo. Hatuwezi hilo kulielewa katika akili zetu lakini huyo ni Mungu asiye na kikomo [1].

Sasa neno kutokuwa na kikomo haliwezi kuvunjwavunjwa chini katika neno la lugha yoyote. Kwahiyo Mungu akiwa asiye na kikomo ni anayejua mambo yote, na anayejua kila kitu kinachoendelea kila mahali na kwa wakati wote lakini yeye mwenyewe ni mtu akiwa anakaa mahali pamoja kwahiyo tunaweza kumuita Yeye ni ajuaye yote. [2].

Mungu ni asiye shindwa na kitu, aliye kila mahali kwa kule kujua kila kitu kunamfanya yeye kuwa kila mahali, anajua mambo yote lakini Mungu hawezi akawa kama hewa ilivyo kwa sababu ana mahali anakaa, Mungu siyo wazo la kuwazia, Mungu ni kiumbe: Mungu, Yesu Yeye Mungu (Kiwakilishi) ni kiumbe kwahiyo anajua yote yapo kila mahali, ni mwenye uwezo wote na hana kikomo. Sasa kuwa asiye na kikomo inatoka kwenye neno asiye na kikomo, ambayo

haina mwisho/mipaka,Yeye ni wa milele, milele ni kama duara inaenda ikizunguka na kuzunguka nawe ukijaribu kutafuta imeanzia wapi ama imeishia wapi, haina mwanzo/haina inapo ishia.Mungu yupo kama almasi kubwa ambayo inakaa kama hivi na vile vipawa vya Roho Mtakatifu **(1Wakorintho 12)** ni kuakisi kwa ile almasi ambayo inarusha mionzi yake kutoka kwenye ile almasi kubwa kama vile vipawa tisa vya kiroho katika kanisa ni kama miale tisa ambayo Roho Mtakatifu anaiakisi ndani ya kanisa.ni nuru ya ajabu gani kutembea ndani yake ambayo inatoka kwenye ile almasi kubwa ambayo ni Mungu [3].

Ufahamu wake mkuu wa kimbele unawaambia haya mambo yote kwa ufahamu, kwa maarifa ya kimbele.Yeye ni aliye kila mahali, kwa sababu anajua kila kitu, Anajua kila kitu kwasababu yuko kila mahali. Kwa hiyo maarifa yake ya kimbelesasa hawezi akawa kama kaupepo juu ya dunia kwa sababu kweli yeye ni kumbe.Yeye sio wazo la kuwanzia yeye ni kiumbe yeye ana mahali anapo kaa tena anakaa katika nyumba **(Isaya 66:1-2)** anakaa mahali panapoitwa Mbinguni na kwahiyo kwa uwezo wake wa kuwa kila mahali akiwa anajua yote akijua vitu vyote hapo sasa yeye yupo kila mahali kwasababu anajua vitu vyote [4].

Yeye alijua hakai kwenye nyumba zilizojengwa na mkono **(Matendo 7:48)** na pengine hapa katika Isaya **(Isaya 66:1)** alisema mwili umeniandalia mimi sadaka na matoleo na majengo na kadhalika.(hivyo hukutaka) lakini ni mwili umeniandalia mimi **(Waebrania 10:5-6)** vema tunatambua kwamba Yeye alikuwa akizungumzia mwili ambapo Mungu angekaa ndani ya **Kristo ,(Yohana 2:19-21)** [5]

Yeye alikua ni Mungu mtu, alikua ni Mungu, Kiungu,amezaliwa na bikira. Mungu Jehova, alimfunika bikira mdogo akamleta mwana wa Mungu aliyezaliwa kibikira **(Isaya 7:14)** na hiyo ilikuwa maskani au mahali alipokalia Jehova mwenyewe.Jehova alitembea katika maskani ya nyama na akalipa gharama ya dhambi **(2 Wakorintho 5:18:19)** msimuache yeye awe nabii, Yeye alikuwa ni Mungu wa nabii? Hakika alikuwa hivyo Yeye alikua zaidi ya mtu mzuri, yeye alikua ni Mungu wa watu wazuri. [6]

Sasa Mungu alimpa Kristo Yule Roho bila kipimo **(Yohana 3:34)** Hiyo ni sahihi! Ukamilifu wa Mungu ulikuwa ndani ya Kristo **(Wakolosai 2:9-10)** Alikuwa ni Mungu Emanuel tunajua hilo, hatuna shaka katika akili zetu juu ya hilo. kama vile nilinyo sema “Bahari iliyojaa maji , maji yote yaliyokua baharini yalikuwa ndani ya Kristo lakini huyu msichana mdogo unayemuona akifanya kazi hapa ni mtu mdogo tu kama hivyo tu kijiko kimekaa pale kama tone naweza kuliona lakini katika Kristo ulikuwa ni utimilifu wote wa Mungu sisi tunaye kwa sehemu. **(Rum 12:6)** alikua naye bila kipimo. Biblia ilisema hivyo unaona? Bila kipimo hakuna njia, yeye ni asiye na kikomo alikua na Roho wa Mungu. Sasa siku moja wakati Mungu anajua Roho wake alikua ndani ya Kristo kwa utimilifu wote, alitaka atumie kipawa chake kilicho ndani ya mtu. Ule mwili wa binadamu uliitwa Yesu ambapo ndio mahali pake alipokua anakaa,ule mwili ulikuwa ni maskani ya Mungu alikua anakaa hapa duniani. Je unaliadini hilo? Wapendwa? Katika mwili wa Kristo **(1Yohana 1:3,14-18)** [7].

Tunafahamu kwamba katika agano la kale chini ya sheria ya Musa kila asomaye anajua hilo kwamba kulikuwa na vyumba vitatu na mapazia mawili katika ile maskani ya Mungu iliyokuwa jangwani (Hesabu 7:89) na (Kutoka 25:22: kutoka 33:7-31) ya kwanza ilikuwa sehemu iliyokua inakaa mkusanyiko halafu mahali patakatifu halafu patakatifu patakatifu hiyo ni nyumba ya

Mungu. Hapo ni mahali anapokaa Mungu. (**Kutoka 40:34-38**) Hapo ni mahala pako pa kukalia sasa unaishi katika nyumba ya vyumba vitatu tu kumbuka unaweza ukawa na vyumba viwili vya kulala, unaweza ukaka na majiko, unaweza na majiko matatu lakini unaishi nyumba ya vyumba vitatu tu.

(**1Thethalonike 5:23-24**) Mungu aliishi katika nyumba ya vitatu alipokua hapa duniani, alikaa katika nyumba ya vyumba vitatu nafsi, mwilini, na Roho ya Yesu Kristo [8].

Sasa hapa angalia kilichotokea oho! Hili linaniweka mahali hasa ambapo nina papenda unaona? Yule lagos na hii chemchem kuu, hii chemchemu kuu ya Roho ambayo haina mwanzo wala mwisho huyu Roho mkuu alianza kujiumba katika huu umbaji. Na huyu Logos ambaye alitoka ndani yake aliitwa mwana wa Mungu. Ilikua ni sehemu pekee inayonekana ya yule Roho aliyokua nayo na ilikua siyo fani ikimaanisha mwili Musa aliona pale ilipopita kwenye mwamba (**Kutoka 33:19-23**) naye akaiangalia akasema inaonekana kama sehemu ya nyumba ya mwanaume. Ni aina ya mwili ambapo tunapokuta nyumba hii ya udongo ikiharibika tunayo nyumba inayotungojea tayari (**2 Wakorintho 5:1**) hiyo ndiyo yenywe na hiyo ndiyo thiolani ambayo ilikua mwana wa Mungu yule mwana, yule Logos akafanyika mwili kwasababu uliwekwa katika mwili ile thiolani yule akafanyika mwili (**Yohana 1:1-2-14**) apa miongoni na alikua chochote isipokua ni mahali pa kukaa mahali pakukaa kwajili ya ile chemchem yote iliyokaa ndani yake (**Wakorosai 2:9-10**) oh! Unaliona hilo hilo hapo? [9].

Sasa katika (**Mathayo 28:18**) tunasoma aya baada ya kusulubiwa kwake akafufuka siku ya tatu alikutana na wanafunzi wake akawaagiza waende ulimwenguni kote kuhubiri injili kwa kila kiumbe akasema “ Nimepewa mamlaka yote mikononi mwangu mbinguni na duniani. Mamlaka yote ya mbinguni, Mamlaka yote ya Duniani nimepewa Mimi”. Ilikua ni nini? Mtu na Mungu wameungana yule logos amefanyika mwili naye ameuwawa na akafufuka tena kwa kuhesabiwa haki kwetu naye amekua Emanuel mpkwa mafuta milele na milele (**Mathayo 1:21-23**) Mungu alibadilisha makao yake kutoka kwenye kiti chake cha enzi kilichoko hewani huku ng'ambo na kukiweka kwenye wa mwana Kristo Yesu kuishi na kutawala milele “Mungu alikua ndani ya Kristo” (**2 Wakorintho 5:18-19**) Yeye ni mahali pa kupumzikia pa mwisho pa yule Roho. Yule Roho alikaa katika maskani siku moja unajua hilo chini ya hema “ Na Suleimani alimjengea yeye nyumba (**2 nyakati 5**) lakini vipi yeye aliye juu hakai kwenye nyumba zilizo jengwa na mikono ya wanadamu” “Lakini mwili umeniandalia mimi” katika kitabu cha matendo ya mitume 7:44-50 wakati Stephano aliposema, “Yote hayo aliyaona kimbele Musa alimjengea hema alikua na hema na akaweka lile sanduku la agano pale kwasababu Mungu alikua pale kwenye kiti cha rehema hakukaa pale vizuri” “ mwili umeniandalia mimi’ mwili wa Yesu Kristo uliofunga mdogo kuliko malaika ili kuonja mauti. Si mwingine bali yeye aliye juu kuliko yoyote aliye juu Kristo. Mfalme wa Omani, Mfalme wa wafalme, Bwana wa mabwana, Muumba kila nyota katika ulimwengu [10].

Yule Baba alikua ni Jehova mkuu Mungu aliye kaa katika maskani inayoitwa Yesu Kristo ambaye ni mwana wa Mungu aliyepakwa mafuta. Yesu alikua mtu na Mungu ni roho na hakuna aliyemuomba Mungu wakati wote lakini mwana peke wa baba amemzihirisha yeye.

(**Yohana 1:8**) nafsi yake utu wake. Uungu wake chochote alichokua alikua ni Mungu. Hakuna chochote kilichopungua wala chochote kilichozidi Mungu. Bado yeye alikua ni mwanadamu

alikuwa mwanadamu. Nyumba ambayo Mungu alikaa ndani yake alikua ni mahali alipokalia Mungu [11].

Ile maskani ni nini. Sasa mwili Mungu akikaa kwenye mwili, Mungu wakati mmoja alikua juu alipokuja katika mlima Sinai, Hata kama dume la Ng'ombe au ng'ombe akigusa ule mlima ilibidi lazima auawe. Mungu ni mtakatifu (**Kutoka 19**) sasa Mungu mtakatifu asingevumilia dhambi kwa hiyo hakuna chochote ambacho kingegusa ule mlima mahali alipo Mungu. Ndipo Mungu akafanyika mwili na akakaa kwetu katika umbo la Yesu Kristo mwana wake. Uumbaji wake, halafu yule mwana akatoa maisha yake na chembechembe za damu ya Mungu zilivunjwa ili uhai utoke kwenye damu uje kwetu (**Yohana 19:31-34**) kupitia hiyo damu tunatakaswa. Uhai wetu (**Rumi 8:3-4**) ambao ulitokana na kujuana kimwili kwa tama uliuleta uhai wetu duniani. Damu ya Yesu Kristo inatuosha sisi (**Waraka 1 Yohana 1:7**) inabadilisha asili yetu kwa kumtuma Roho Mtakatifu kwetu tunakua katika asili ya Mungu (**2Petro 1:7-4**) Sasa tunakua kao la kukaa Mungu [12].

Mungu alitabiri kupitia manabii akisema “Nitaziandika sheria zangu katika mioyo yao mahali nitakapo ziweka katika meza za mioyo yao”.

(**Waebrania 8:10-13**) kuonyesha kwamba hiyo itakua ni mahali pa Mungu pa kukalia katika moyo wa mwanadamu sio katika kichwa cha mwanadamu lakini katika moyo wa mwanadamu Amina.

“Nitaziandika hizo katika mioyo yao nao watashika maagizo yangu” asema bwana. Mungu alisema hivi katika mahali fulani katika (**Ezekiel 36:24-28**) alisema “katika siku ile nitaona moyo wenu wa jiwe, nitawapa Roho mpya na kuweka Roho yangu ndani yenu”. Sasa watu wengi hata ninyi watu wa kipentekoste mnaifanya makosa katika hilo. Mnapata Roho mpya, hiyo sio Roho ya Mungu. Hiyo ni wewe sio Mungu unapata furaha kidogo sababu una Roho mpya na unaruka juu na chini unakimbia hapa na pale na pengine unapiga kelele kidogo unazungumza kwa lugha ukifikiri umepata Roho mtakatifu. Hiyo siyo, hiyo ni Roho mpya Mungu amekupa wewe hiyo ni wewe. Angalia unapata Roho mpya, Mungu inabidi akupe wewe Roho mpya. Vinginevyo usingeweza kuelewana nae. Wewe mwenyewe huwezi ukaendelea vizuri wewe mwenyewe ila Roho ya shetani ya zamani uliyokua nayo. Kwa hiyo ilibidi aweke Roho mpya ndani yako ili uweze kukubaliana na Roho wake. Amen “Nitaweka Roho mpya ndani yao na kuweka Roho yangu ndani yao” Baada ya kukupa Roho mpya ambayo ni wewe usiichanganye na Roho wa Mungu sio. Ni Roho yako mpya ili uweze kwenda vyema na Roho Mtakatifu kama ataenda kukupa Amen. Kwa sababu wewe katika hali yako huwezi ukaenda vizuri, huwezi ukaenda vizuri na mke wako, huwezi kwenda vizuri na mume wako wala jirani yako. Utawezaje kwenda vizuri na Mungu? Kwa hiyo inabidi akupe Roho mpya. Kabla hujaenda vizuri na yeye. Kwa hiyo anaweka Roho mpya ndani yako anaweka Roho yake ndani yako anakupa Roho mpya. Muonekana mpya, Imani mpya. Halafu anaweka Roho Mtakatifu ndani yako (**Waebrania 3:1-6**) [13].

Suala la dhambi linakua limemalizika wakati Roho Mtakatifu anapokuja katika moyo wa mwanadamu (**Waebrania 10:2, 1 Yohana 5:18**) inatupa hoja zote, inaenda juu ya mawazo yetu ya kiakili. Sasa leo sababu watu wengi wakidini leo wanaanguka na kusimama ni kwa sababu ya uelewa wakiakili wa Kristo. Kwa maneno mengine. Kristo yuko akilini mwao sio moyoni

mwao. Unaona hilo wanaliamini tu kiakili na akili yako itahoji. “Inaweza ikawa hivyo? Je uponyaji wa kiungu unaweza kua hivyo? Je ubatizo wa Roho mtakatifu unaweza kua hivyo?” Sasa hivyo ni hoja za kiakili, lakini hilo linapokuja moyoni ni Imani (**Warumi 10:8-13**) ni kitu cha uhakika hakuna swala katika hilo imemalizika milele liko moyoni mwako na moyo wako hauna hoja kwa sababu ni kiti cha enzi mahali anapokaa Mungu katika moyo [14]

Roho Mtakatifu atafanya kila hatua iwe kama Kristo na itakufanya wewe kua kama Kristo. Tunda la Roho ni Upendo, Amani, furaha, uvumilivu, utu wema, upole, subira, wema na Imani. (**Wagalatia 5:22**) haya mambo ndiyo ambayo Roho Mtakatifu Ana ya tawala misisimko yetu sio tu kuruka juu na chini unaweza ukafanya hivyo. Hata densi linaweza likakuletea hayo. Lakini Roho Mtakatifu anakuleta wewe kwenye utawala au utendaji wa Mungu, kwamba unatembea kwa amani na ndani ya upendo na furaha kwa uvumilivu. Utu wema, unyenyekevu, upole, subira. Unaona? Sio kitu unachokifanya mwenywe ni kitu ambacho Roho Mtakatifu anakifanya ndani yako. Unaona? Sio tena kwa mawazo yako mwenywe ya akili, ni kwa ufahamu Utendaji kazi wa Roho Mtakatifu. Oh! Laiti ningeweza kupaza sauti kumsifu Mungu Duniani kote.

Kanisa la Mungu aliye hai, hapo ndipo kanisa la Kipentekosti liliposhindwa, kuna muziki uliofanywa na wanadamu, kupiga makofi, kuruka juu na chini, msisimko. Wakati kama tungerudi huko mitaani na Roho Mtakatifu ikiwa hatawali maisha yetu ni kuhusiana na hilo, hatuna Roho Mtakatifu. Hayo siyo maziwa ya mtoto lakini, ndugu hicho ndicho kanisa linachohitaji. Uzima pekee unaweza kuja kwa Roho Mtakatifu [15].

Kanisa hivi sasa linapaswa liwe limechukua nafasi ya Yesu Kristo kuendeleza huduma yake, “Yeye aniaminiye Mimi kazi nizifanyazo naye atazifanya, hata hivyo bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona lakini ninyi mtaniona kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi hata ndani Yenu mpaka ukamilifu wa dahari” unaona? Hilo hapo, kuendeleza kazi zake (**Yohana 14:12-19**).

Mungu anakaa ndani katika ukamilifu wa mwanadamu akijiakisi mwenywe ndani ya hicho kiumbe. Ibada kamilifu! Mungu ndani katika ukamilifu wa mwanadamu akijiakisi mwenywe ndani ya hicho kiumbe ibada kamilifu! Mungu ndani yetu tukiwa maskani yake, Mungu akijidhihirisha kwahiyo, unaona, sote tunajaribu kulifikia. Mahali pa kukaa, Maskani ya Mungu aliyehai (**2Wakorintho 6:16**) Amelinua kanisa lake juu, anawaleta watu wake juu. Nakisha Petro hapa anasema kwanza mambo saba: Imani ni nguvu, (unaona inavyopanda juu) maarifa, subira, utauwa, upendano wa ndugu ongeza upendo wa ndugu kisha upendo wa Mungu; Yule Roho Mtakatifu, Kristo wa kweli wa Roho Mtakatifu, Na ana hizo sifa zote zimetiwa muhuri ndani yako. Kisha, Mungu anaishi ndani ya maskani ambayo inaitwa jengo maskani iliyo hai na ni mahali pakukaa Mungu aliye hai (**2Petro 1:3-11**), (**1Wakorintho 3:6-17**) (**1 wakorintho 6:19-20**). Ongeza katika imani yako nguvu; na katika nguvu zako maarifa na katika maarifa yako sabira, na katika subira yako na katika subira yako, utauwa, na katika utauwa wako, upendano wa ndugu, na katika upendano wa ndugu, Yule Roho Mtakatifu wa Kristo atakuja kwa sababu hapo chini yake yeye yule Roho Mtakatifu ni Roho wa Yesu Kristo kanisani akidhihirisha hizo sifa.

Sasa hiyo ni nyumba ambayo Mungu ana kaa ndani yake siyo jengo na kengele kubwa ndani yake na mnara mrefu lakini “Mwili uliniandalia mimi” Mwili ambao Mungu anaweza kukaa ndani yake. Mungu anaweza kutembea ndani yake, Mungu anaweza kuzungumza ndani yake,

Mungu anaweza kutenda kazi, chombo kilicho hai cha Mungu. Mungu akitembea kwa miguu miwili ndani yako, Utukufu. Hatua za wenye haki huongozwa na haki huongozwa na Mungu akitembea ndani yako kwasababu wewe ni waraka uliokatibiwa ndani usomwao na watu wote **(2 Wakorintho 3:1-3)** na kama uzima /uhai uliokua ndani ya Kristo uko ndani yako, utazaa uhai ambao Kristo alizaa [12].

Sasa watu wengi wanasema kwamba, “Mimi nitaenda mbinguni kwa sababu imani yangu inaniambia hivyo, Mimi ni wa kanisa la imani yangu inaniambia niko sahihi.”

Sasa ninaamini kuhusu neema ya Mungu pia lakini tazama haijalishi imani yako ikoje hutenda hukumu kwa imani yako; utaenda kuhukumikiwa kwa kazi zako **(Yakobo 2:24-26)** na unapokufa kifo kinabadilisha tu nyumba kwa ajili yako na ukifa katika dhambi zako, utaenda kwenye wenyeji mbaya kuliko unaoishi hivi sasa. **(Luka 16: 19-31)** Lakini ukifa katika Kristo utakua pamoja na Kristo kwa sababu yeye ni njia **(Wafilipi 1:21-24)** [16]

Na kumbuka utakapokufa na nafsi kukuacha wewe haibadiliki hapana, bwana, Mauti haibadilishi nafsi inabadilisha mahali pakukaa lakini bado ni nafsi ileile kwa hiyo kama sikuzaliwa mara ya pili na sehemu ya Roho wa Mungu wa milele ilikua na mwanzo. Chochote chenye mwanzo kina mwisho, Hivyo ndiyo sababu Mungu ndiye kitu pekee cha milele ilikua na mwanzo. Chochote chenye mwanzo kina mwisho, Hiyo ndiyo sababu Mungu ndiye kitu pekee cha umilele isipokua umezaliwa mara ya pili na kuwa na uzima wa milele **(Yohana 5:24)** (Neno la kiyunani ZOE) Hapo inamanisha “uzima wa Mungu mwenyewe ndani yako”), utaangamia lakini wakati uzima wa Mungu undani yako huwezi kuangamia kwa vile Mungu asiyoweza kuangamia kwa sababu wewe ni mwana wa Mungu chipukizi la Mungu na una uzima wa milele **(Warumi 8:12-17)** oh! Hicho ndicho kitu kanisa linahitaji kisha wakati Mungu yu ndani yako na Yeye huishi maisha yake mwenyewe kupitia kwako unaona? Na hivyo ndivyo jinsi tunajua kwamba sisi ni wakristo. Hapo unahusika kuhusu ndugu yako. [17]

Wanaume na wanawake ni wakati wa kujitikisa wenyewe na kujipima wenyewe kuona wapi tumesimama, kwakua kifo hakibadilishi. Musa na Eliya walikua wameondoka kwa miaka elfu mbili; karibu miaka elfu mbili na mia tano na hapo wamerudi wakiwa na asili ileile wakifanya mambo yale yale **(Mathayo 17:1-8)**. Mauti haimfanyi kitu mtu wala haibadilishi imani yako wala chochote ndani yako ila makao yako **(Yohana 14:1-5)**.

Kama wewe unashuku neno la Mungu utakua mwenye kushuku upande ule. Sijali umtakatifu kiasi gani namna unavoishi na jinsi maisha yako yaliyo mema haitakubadilisha hata kidogo unapokufa inabadilisha tu makao yako na kama huwezi kulikubali neno lote la Mungu kama lilivyoandikwa hutafanya hivyo huko, kwahiyo usijali hutakuwepo huko. Inabidi ulikubali katika ukamilifu katika nguvu za kuthibitisha kwake na ufunuo wa kile ulicho, kisha unakua sehemu yake. Ni neno lake tu ndilo atakalo liinua kama alivyofanya katika ileile asubuhi ya kwanza ya pasaka. Neno lake tu ndilo linalokuja na wale tu waliyo kufa katika neno lake wakiliamini neno lake kuthibitisha neno lake.

Nukuu

- [1]. Huyu melkizedeki ni nani “(65-0221E) par 48-49
- [2]. Kuweka Wakf “(58-0221E) Par E-5
- [3]. Tangu mwanzo haikua hivyo “(60-0306) par E-10
- [4]. Mambo yatakavyokuako “(60-1205) Par 37-38
- [5]. Ni nyumba gani mtakayo ni jengea “(65-1121) Par 21
- [6]. Kufufuliwa binti Yairo (56-0731) Par E23
- [7]. Ripoti ya safari ya india (57-0126B), Par E58
- [8]. Maisha yaliyofichika (55-1006A), Par F 25
- [9]. Waebrania suraya 1. (57-0821), Par 129-130
- [10]. Waebrania sura ya 2: sehemu ya pili (57-0825E), Par 121-124
- [11]. Maswali na majibu waebrania sehemu ya pili (57-10002) Par 435,439
- [12]. Kimo cha mtu mkamilifu (62-1014M) Par 69-74, 75-77,84,341,451,346.
- [13]. Pazia la ndani ya (56-0121) Par E 59-60
- [14]. Uthibitisho usiashindwa wa kufufuka (57-0114), Part 32
- [15]. Nini kinachohitajika kufanya maisha ya Kristo? (57-0113)
- [16]. Tuende kwa nani? (60-0606) Par E17
- [17]. Kushawishika kisha kuhusika (62-0118) Par 52
- [18]. Tambua siku yako na ujumbe wake (64-0726) Par 68-70

Jiwe la kiroho la kujengea na. 18 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, Yamekusanywa na Gerd Rodewald
friedenstr. 69 D-75328 Schomberg, Germany Simu (+49) 72357613 Fax: (+49) 72353306

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itazunguka dunia. Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyokusudiwa kimbele imesikia.
(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)

Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:

*Charles E. Y. Kanju,
Box 553 Korogwe - Tanga
E-mail: Chaelika@livel.com
Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*

